**102/3**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA TATU**
**FASIHI**
**JUNE 2022**

**MTIHANI WA PAMOJA WA KASSU**
**FASIHI YA KISWAHILI**
**KARATASI YA TATU**
**102/3**

for more free exams visit www.freekcsepastpapers.com

# MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA

*© KASSU JET 2022*

1. **USHAIRI**

(a) Shairi huru (kimapinduzi). Halizingatii arudhi za utunzi.

(b) (i) kuwepo kwa mishororo

(ii) kuwepo kwa beti

(iii) matumizi ya lugha ya mkato

(iv) vina vinajitokeza kwa kiwango fulani

(c) (i) inkisari (kufupisha kwa maneno) km. Mlokabili badala ya mliokabili, zilokumba badala ya zilizokumba, mlohimili badala ya mliohimili

(ii) kuboronga sarufi/kufinyanga sarufi – niarifu zenu idhilali badala ya niarifu idhilali zenu,, nileteeni yenu matambara – nilteeni matambara yenu

(iii) tabdila – mikitaba – mikataba, majutuhi - majeruhi

(d) Mateso na dhiki zinazowakumba maskini –ya dhiki ya maskini kumpelekea Manani

Hali duni ya maisha licha ya kujibidiisha kazini – matambara

Hatari katika kufanya kazi – nyavu zilizokumba hatari, na nguvu za mawimbi mlohimili

(e) Takriri- leteni nyavu ..., nileteni yenu matambara leteni

(f) Msimulizi anasema anaunda mikataba ya dhiki za maskini ili amplekee Mungu, lakini hofu yake kubwa ni kuwa huenda ikatukia kuwa Mungu hajui kusema – anachelea hilo

**(g) <u>Mizani</u>**

| Ubeti wa kwanza | ubeti wa pili |
|---|---|
| 9 | 9 |
| 10 | 12 |
| 14 | 12 |

**Mishororo mitatu katika kila ubeti**

**<u>Vina</u>**

Vina vya mwisho

| <u>Ubeti wa 1</u> | <u>Ubeti wa 2</u> |
|---|---|
| -li | -ri |
| - li | - ri |
| - li | - li |

for more free exams visit www.freekcsepastpapers.com

**CHOZI LA HERI**

2 (a)… haya imekuandama tangu usiku ukimtongoza fulani; siku za kuchora ramani ya Afrika kwa vyanda vya miguu, hadi sasa? Ama ni hizo mvi unaficha? Naskia ile mid-life crisis ikiwashika wazee ndiyo hivyo;

i) Weka dondoo hili kwenye muktadha wake. (Alama 4)

Msemaji ni **Terry mawazoni mwa Ridhaa**
Msemewa ni **Ridhaa**
Ridhaa **yuko kwenye mawazoni uwanjani wa ndege wa Rubaa**
Anakumbuka Maisha yake mkewe na aila yake huku akimgojea mwanawe **mwangeka anayetoka ng'ambo**

ii) Tambua mbinu zozote tatu za kimtindo kwenye dondoo hii (alama 3)

Taswira(mwono) kuchora ramani ya Afrika

Maswali ya balagha. Hadi sasa? Ama ni hizo mvi unaficha?

Kuchanganya ndimi. Mid-life crisis

Mbinu rejeshi/Kisengere nyuma – Ridhaa kukumbuka yaliyopita

iii) Jadili sifa zozote tano za msemewa (alama 5)

Sifa za **Ridhaa**
**mwenye bidi-** alifanya kazi zake kwa bidi hospitalini
**mvumilivu-** hata baada ya familia yake kufa na mali kupotea, alizidi kuvumilia hali hiyo mpya ya ukiwa
**mwenye mapenzi-** anaipenda aila yake na hata selume rafikiye.
**Mshauri mwema-** anaonekana kumshauri mwangeka mwanawe aoe na ajenge Maisha yake upya
Kadiria hoja ya mwanafunzi hapa. 1 x 5

(b) Dhibitisha kauli kwamba **'kweli jaza ya hisani ni madhila'** kwa kurejelea wahusika **wanane** kwenye riwaya ya chozi la heri. (Alama 8)

Ridhaa aliwatendea hisani wahafidhina kwa kupanda miti kwenye Kijiji na kusambaza maji ya mabomba, hatimaye alichukuliwa kama mgeni mahali hapo hata kuchomewa mali yake na familia yake kuuawa.

Selume hata baada ya kumpenda mumewe na kuishi vyema na wakweze, anafukuzwa nyumbani kwa kutofautiana nao kwa misingi ya kisiasa na kujipata kwenye msitu wa mamba.

Makaa- alijitolea mhanga kuwaokoa wananchi waliokuwa wakifyonza mafuta kwenye lori iliyoanguka. Mshahara wake ulikuwa kifo cha uchungu.

for more free exams visit www.freekcsepastpapers.com

Lunga alitetea haki za wananchi wasije wakanunuliwa mahindi mabovu na muishowe akapigwa kalamu kazini.

Mwekevu aliwajengea wanachi visima katika sehemu zilizokuwa na ukame. Hatimaye walimsaliti kwa kusema hawawezi kuongozwa na mwanamke na nuishowe kupigana na kusababisha maangamizi makubwa.

Kiriri alijizatiti kuwasomesha wanawe ugaibuni na hata mkewe, baadaye familia hiyo walikataa kurejea nyumbani na kumsabaishia kihoro akafa.

Billy alimjengea Sally kijumba ili waishi raha mstarehe, alipompeleka aone jumba, aliambiwa kuwa nyumba hiyo ilikuwa kama kiota cha ndege.

Babake Tuama alimshauri bintiye kutokeketwa na badala yake Tuama alikeketwa na kujipata katika hali mbaya hospitalini na kumsabishia aibu babake.
Zohari- baada ya wazazi wake kumkimu kwa mahitaji yake yote hadi kumpeleka shuleni, alijiingiza kwa mapenzi ya kiholela na kusababisha mimba ya mapema. Baadaye anaalifukuzwa shuleni na akatoroka nyumbani.

Kadiria majibu. (Hoja moja kwa kila mhusika) 8 x 1

for more free exams visit www.freekcsepastpapers.com

3.
a) **Vita:** baada ya vita vya baada ya uchaguzi, mapigano hayo yalifika mwisho na watu wakaishi Maisha mapya.
b) **Elimu.** Ridhaa alighadhabika alipoitwa mfuata mvua shuleni na mwizi wa kalamu, hatimaye aliweza kusoma hadi kiwango cha chou kikuu.
c) **Ukosefu wa ajira**- shamsi alisoma na kuwa jogoo wa kwanza musomi kwenye Kijiji chao, hatimaye anasikika akinungunikia kutoajiriwa kwenye wimbo wake.
d) **Changamoto za ndoa-** Naomi hata baada ya kuishi na mumewe na kujaliwa Watoto, hatimaye anawaacha na kupotea asijulikane aliko.
e) **Ubakaji-** wanawe kaizari lime na mwanaheri wanabakwa huku babake akiona na mwishowe wanayajenga upya Maisha yao.
f) **Dhulma za wanadamu**- Dick anabadilika baada ya kutekwa nyara na kutumiwa kuuza dawa za kulevya.
g) **Mauaji-** familia ya ridhaa wanauawa kw na kuchomeka kiasi cha kutoatambulika kwa sababu ya ukabila.
h) **Uharibifu wa mali-** waandamanaji walipora maduka na vijana wakachoma magari kwa mabomu ya petroli kwa gadhabu waliokuwa nayo baada ya uchaguzi. Yote yakaisha na watu wakarudi sawa.

i) **Utengano –** Dick, Umu na Mwaliko walikutana mwishowe.

j) **Ukiukaji wa haki za Watoto**- Sauna anawauza Dick na Mwaliko kwa Buda badala ya kuwatunza. Buda anawafundisha namna ya kuuza dawa za kulevya. Sauna akashikwa na kufungwa.

k) **Umaskini;** Kangata na mke wake Ndarine waliishi msitu wa mamba kwa muda murefu kwani hawakuwa na makwao. Waliishi kwa shamba ya mwajiri wao aliyeishi mjini. Mwishowe wakamiliki ardhi.

**Hakiki** **Hoja zozote 10 x 2 = 20**

**Tamthilia**

(a) **4** Vipengele vya kimtindo

- Chuku- alizaliwa na meno mdomoni
- Siyahi/nidaa- Kisirani huyu!
- Balagha- wataka kuniharibia siku yangu nile nini?
- Tashbihi- wadhani nauza nyonga kama huyo Tunu wako?
- Ulinganuzi- kuna hali ya kulinganua watu wawili mfano: Wafikiri nauza nyonga kama huyo Tunu wako?
- Mdokezo- Nita...
- Kejeli- sijui watetezi wa nini watawatetea
- Kinaya- Nanyi mheshimu uhuru wenu- ni kinyume cha matarajio kwa vile watu hawana uhuru unaorejelewa bali wanatawaliwa kiimla na Majoka.
- (**Hoja za kwanza 6x1=6**)

(b) Mandhari

Mangweni- hapa ni mahali shughuli za utengenezaji na unywaji wa pombe haramu zinafanyika. (1x2=2)

for more free exams visit www.freekcsepastpapers.com

(c) Jinsi mandhari yanaendeleza usimulizi wa hadithi. (alama 12)

- Kuonyesha jinsi baadhi ya wanajamii walivyozamia katika shughuli za **anasa**.
- Kuonyesha **madhara ya ulevi**. Sudi anasema, "Hatujaja hapa kuchoma mafigo yetu bwana" uk 57. Aidha pombe inasababisha upofu na vifo.
- Kuashiria **mabadiliko** katika maisha ya mhusika- Tunaelezwa kuwa awali, Siti alikuwa mnywaji wa pombe haramu. (uk. 58)
- Kuonyesha jinsi uongozi unatolewa kwa misingi ya **kinasaba**. Ngurumo anamuuliza Tunu yeye ni nani, babake au babuye walikuwa nani Sagamoyo.
- Kuonyesha juhudi za **wapiganiaji uhuru**. Sudi anasema mashujaa halisi ni wale waliowahangaisha wakoloni hata wakawatimua. (uk. 58)
- Kuonyesha **utepetevu** masomoni- Ngurumo anasema hakulipenda somo la Historia.
- Kuonyesha **ubarakala**- Ngurumo anasema kura yake hampi tunu heri ampe paka.

- Kuonyesha jitihada za **wakombozi.** Tunu anawaeleza walevi pale mangweni kuwa wamefika hapo ili kuwaalika kuhudhuria mkutano nje ya lango la soko la Chapakazi. (uk. 59)
- Unywaji wa pombe unasababisha **utegemezi**- Ngurumo anasema watu wa kigogo wao wakipitia mangweni hawakosi kuwapa kitu kidogo. (uk. 60)
- Kuonyesha **kutamauka**- baada ya soko kufungwa, watu wanahamia mangweni ili kujiliwaza. (uk. 61)
- Utawala kuidhinisha utengenezaji na ulanguzi wa **pombe haramu**. Kwa kufanya hivi ni kwenda kinyume na sheria za jimbo lao. (uk. 61)
- Kuonyesha **uzinifu**. Ngurumo ana uhusiano wa kimapenzi na Asiya ambaye ni mkewe Boza. (uk. 64)
- **Kudhalilishwa** kwa mwanamke- Ngurumo anawaongoza walevi wengine kuimba wimbo wa kumkejeli Tunu. (uk. 65)
  **(Hoja zozote 6x2= 12)**

**5.**

a) Weka dondoo katika muktadha wake. (Alama 4)
   i) Msemaji ni Tunu.
   ii) Msemewa ni Sudi.
   iii) Wako nyumbani kwa Sudi (barazani).
   iv) Tunu anajaribu kumshawishi Sudi waendelee na harakati za ukombozi Sagamoyo.

b) Fafanua hulka nne za msemewa <u>zinazojitokeza ndani ya muktadha</u> huu. (Alama 4)
   i) Bidii – Licha ya kufungwa kwa soko la Chapakazi walikofanyia kazi, anaendeleza juhudi za uchongaji vinyago barazani mwake.
   ii) Mzalendo –Anaitikia wito wa Siti kwenda kwenye shughuli za maandamano walikouawa vijana tano. Anahimiza waende bila kuchelewa.
   iii) Ni mlezi mwema – Anamtuliza mwanawe Pili na kumhakikishia kuwa atampa chakula.
   iv) Ni mwenye mapenzi kwa wanawe – Anaijali hali ya wanawe. Anamkumbatia Pili na kumpa ahadi ya kumpa chakula.
   v) Ni mwenye kukata tamaa – Anaelekea kukata tamaa ya kushiriki kwenye harakati za ukombozi. Anaona kama hili linamzuia kuwajibikia riziki ya familia yake.

c) Onyesha msemaji alivyofanikiwa katika azma yake ukirejelea tamthilia zima. (Alama 12) (Alikuwa na azma ya Kulinda uhai. Kulinda haki. Kulinda uhuru n.k )
   i) Anafaulu kutoa <u>suluhu kwa njaa</u> iliyowakaba wanawe Sudi. Anasema wapelekwe kwao mama yake angewalisha na kuwatunza.
   ii) Anafanikiwa <u>kumshawishi Sudi</u> waendelee na harakati za ukombozo wa Sagamoyo. Hii ni licha ya Sudi kutaka kukata tamaa.

for more free exams visit www.freekcsepastpapers.com

iii) Akiwa chuoni, alipata mafaniko katika mapambano ya kutetea haki akiwa kiongozi wa wanafunzi.
iv) Aliazimia kusomea sheria chuoni na akafanikiwa kusoma hadi kiwango cha uzamifu.
v) Anafaulu kumkabili Majoka ana kwa ana ofisini mwake. Anatumika fursa hiyo kumwambia Majoka kuhusu mapungufu ya uongozi wake k.v kuendeleza mauaji.
vi) Anafaulu kupinga ujenzi wa hoteli ya kibanafsi kwenye Soko la Chapakazi. Majoka alinuia kujenga hoteli hiyo baada ya kuvibomoa vibanda vya soko.
vii) Anafanikiwa katika juhudi za kutaka soko lifunguliwe. Anaongoza mkutano unaokuwa kilele cha kulirejesha soko mikononi mwa wanasagamoyo.
viii) Azma yake ya kukutana majangili waliomshambulia inatimia anapompata Ngurumo mangweni na kukemea kitendo chake cha kikatili.
ix) Anatimiza lengo lake la kuwazindua wanasagamoyo waliozamia ulevini. Anawahimiza kuijali kesho yao.
x) Anafanikiwa katika kulaani uuzaji wa pombe haramu. Akirejelea katiba ya nchi, anamkumbusha Asiya kuwa ni hatia kuuza pombe haramu.
xi) Anaukemea uasherati katika jamii. Anakejeli 'keki za uroda' zilizookwa na Asiya aliyepata kandarasi kwa kumpa ngurumo uroda.
xii) Anafanikiwa kuongoza maandamano pamoja na wanaharakati. Maandamano hayo yalichapishwa kwenye gazeti.
xiii) Anafanikiwa kuwahutubia waandishi wa habari kuhusu kufujwa kwa pesa za kusafisha soko, kunyimwa haki kwa wauzaji n.k
xiv) Anafaulu kuwa na wafadhili wanaofadhili gazeti linaloandika taarifa kuhusu harakati na kuendeleza harakati za ukombozi Sagamoyo.
xv) Tunu anafikiwa kuzipeperusha habari za uanaharakati moja kwa moja kupitia runinga ya mzalendo na katika mitandao ya kijamii.
xvi) Anafaulu kuwaleta wanasagamoyo pamoja dhidi ya uongozi wa Majoka. Watu waliususia mkutano wa Majoka wakaenda mkutano wa Tunu nje ya lango la soko.
xvii) Anapata nafasi ya kuwatolea hotuba wanasagamoyo nje ya lango la soko. Anawakumbusha wanasagamoyo kuhusu maana halisi ya uhuru wao.
xviii) Anapata mafanikio baada ya kupata uungwaji mkono na mkuu wa polisi Bwana Kingi. Anakubali kuulinda usalama wa waliohudhuria mkutano nje ya lango la soko.
xix) Azma yake ya kupinga kuchaguliwa kwa viongozi wabaya inafaulu. Wanasagamoyo wanaahidi kutowachagua viongozi wa aina hiyo tena.
xx) Tunu anafaulu katika kuinua hadhi ya wanawake Sagamoyo. Anatambuliwa kwa juhudi zake za kuleta ukombozi; Sudi anazindua kinyago chake kusherehekea uhuru wa kweli.

for more free exams visit www.freekcsepastpapers.com

**HADITHI FUPI**

**6. MAME BAKARI**

(a) Muktadha wa dondoo
Haya ni maneno ya Sara katika uzungumzi nafsia.
Anawaza akiwa nyumbani kwao
Anawazia dhuluma ambazo angepata baada ya kubakwa na janadume.

(b) Mbinu za kimtindo katika dondoo
Uradidi/takriri …dunia dunia
Jazanda…dunia ya msumari moto juu ya kidonda
Balagha…hao watu je?
Kadiria. Zozote 2x2=4

(c) Kudhibitisha kauli "Dunia ya msumari moto juu ya donda mbichi"
1.Sara angetengwa,kusutwa na kukashifiwa kwa kosa lisilo lake
2. Babake 'angemchinja'au amfukuze nyumbani
3. Kukosa kuaminika.Sara anahofia babake huenda asimwamini
4. Kufukuzwa shuleni. Sara anahofia kuwa angefukuzwa shuleni
5.Kupata ujauzito. Sara anaambulia ujauzito baada ya kubakwa na janadume
6. Dhiki za kisaikolojia
7. Janadume linapatikana likijaribu kumbaka msichana mwingine,baada ya kumnajisi Sara
**Tanbihi .**Hoja zizingatie masaibu ya Sara baada ya kubakwa. Zozote 6x1=6

for more free exams visit www.freekcsepastpapers.com

(d) Mwanamke alivyosawiriwa katika hadithi.
1. Anadhulumiwa kimapenzi –Sara
2. Anatumiwa kama chombo cha kumridhisha mwanamme
3. Msiri -Sara
4. Mwenye kuwajibika – Beluwa
5. Mwenye busara –mamake Sara
6. Kiumbe dhaifu –Sara baada ya kubakwa
   Kadiria zozote 6x1=6

7. **TULIPOKUTANA TENA**

(a) Mbinu za mtindo

1. Tashhisi/uhuishi …mbavu zikamtafuna
2. Takriri/uradidi…alicheka kicheko
3. Chuku…uliosafiri robo dunia
4. Utohozi… soli
5. Nidaa…magharibi!
6. Taswira.. kicheko cha Kazu

(b) Matumizi ya mbinu rejeshi

1. Sebu anakumbuka habari za rafiki yake Bogoa aliyaletwa kijijini mwao uk108
2. Bogoa alivyopelekwa mjini na babake kuishi na rafiki uk 115
3. Bogoa alivyoishi kwa shida kwa Bi. Sinai uk 118
4. Sebu anakimbuka maisha ya ujana wao na Bogoa uk 119
5. Sebu ankimbuka akimuuliza Bogoa kilichofanyika kwa viganja vyake uk119
6. Jinsi Bogoa na Sebu walivyokuwa wakicheza densi uk 119

   Kadiria zozote 5x1=5

(c) Umuhimu wa Club Pogopogo

1. Eneo la mkutano wa kina Kazu na Bogoa
2. Kazu anakutana na mke wa Bogoa – Sakina
3. Hali ya kiuchumi ya Kazu na wenzake inabainika ( Club ni maarufu kwa watu wa kipato cha chini uk111)
4. Tunafahamu alivyofika mjini Bogoa
5. Ukatili wa Bi Sinai
6. Kifo cha wazazi wa Bogoa na Bi Sinai
7. Kutoroka kwa Bogoa kutoka kwa Bi Sinai
8. Eneo la burudani

   Kadiria zozote 4x4=4

(d) Matatizo ya Bogoa

1. Kutengana na wazazi katika umri mdogo
2. Kukosa elimu
3. Kufanyishwa kazi za kitumwa(**mtahinwa anaweza kuorodhesha zile kazi kama hoja inayojisimamia)**
4. Kunyimwa muda wa kucheza na watoto wenzake
5. Kunyimwa chakula na kupewa makombo
6. Kulia sufuria
7. Kuchomwa viganja

   Kadiria zozote 6x1=6

for more free exams visit www.freekcsepastpapers.com

**FASIHI SIMULIZI**

8. (i) Tambua kipera katika dondoo. (alama 1)

***hotuba***

(ii) Eleza sifa za kipera ulichotaja katika (i) (alama 4)

- ***a) Hutolewa na watu maalum walioteuliwa kuzungumza.***
- ***b) Watu wanaotoa hotuba aghalabu huwa na umilisi mkubwa wa lugha.***
- ***c) Hotolewa kwa nafsi ya kwanza.***
- ***d) Mtoaji hotuba anaweza kutumia viziada lugha kama vile ishara za mikono.***
- ***e) Hotuba huteuliwa mada mahususi wala haizungumzii jambo lolote.***

***Zozote 4 x 1 = 4***

(iii) Eleza dhima zozote mbili za kipera ulichotaja katika (i) (alama 2)

- ***a) Kuwaelimisha wanajamii kwa kuwapa maarifa ya kukabiliana na maisha.***
- ***b) Kuadilisha na kutoa nasaha hadharani.***
- ***c) Huimarisha ukakamavu wa kuzungumza kadiri watu wanavyotoa hotuba hadharani.***
- ***d) Kukuza ufasaha na umilisi wa lugha.***
- ***e) Kupalilia kipawa cha uongozi.*** ***Zozote 2 x 2 = 2***

for more free exams visit www.freekcsepastpapers.com

(iv) Tanzu za fasihi huingiliana na kutegemeana. Thibitisha kauli hii kwa kurejelea kifungu hiki. (alama 6)

Kifungu hiki ni cha hotuba. Hata hivyo, hotuba yenyewe imejumuisha tanzu nyingine za fasihi simulizi kama vile:

- ***a) Kuna matumizi wa nyimbo – wimbo uliotumika unaonyesha jinsi watu walivyojisifu kwa uhodari wao vitani na ngomani.***
- ***b) Hadithi – hadithi inayohusu mwanamke na nyama inarejelewa.***
- ***c) Semi – kifungu hiki kimejumuisha methali na nahau. Kwa mfano, mchelea mwana kulia hulia mwenyewe.***
- ***d) Miviga – msimulizi anadokeza kuhusu tohara kwa vijana kwa kutaja kisu cha ngariba.***

***Zozote 3 x 2 = 6***

(v) Eleza toni iliyobainika katika kifungu. (alama 2)

***Toni ya kushauri – nafsi neni anawashauri vijana waliopashwa tohari na walezi wao.***

***Kutaja 1, kueleza 1***

(vi) Fafanua mbinu za kimtindo zinazodhihirika katika kifungu hiki. (alama 5)

- ***a) Methali – mchelea mwana kulia hulia mwenyewe.***
- ***b) Nahau – kutia bidii***
- ***c) Mbinu rejeshi – nafsi neni anarejelea simulizi ya bibi.***
- ***d) Takriri – ni matendo na tabia***
- ***e) Taswira – vijana wadogo wamelala matopeni; wakitumbuizwa na milio ya vyura***
- ***f) Tashihisi – elimu itawafungulia milango ya heri***
- ***g) Sitiari – elimu ni silaha ya pekee***

***Zozote 5 x 1 = 5***

for more free exams visit www.freekcsepastpapers.com